# UMBO LA MASHAIRI

Kithaka wa Mberia

Kwa muda wa kama miongo miwili hivi kumekuwepo na mabishano juu ya ushairi wa Kiswahili kuhusiana na suala la umbo la mashairi.[1] Mabishano hayo yameshirikisha makundi mawili. Kundi moja la washairi na wataalamu wa Ushairi wa Kiswahili limekuwa liking'ang'ania na lingali lang'ang'ania kwamba kuna masharti mahususi ambayo ni lazima yafuatwe na kila mashairi. Matokeo ya kutimizwa masharti haya ni umbo maalum la mashairi. Msimamo huo umepingwa sana na kundi la pili ambalo lashikilia kwamba hakupaswi kuwepo na umbo maalum la mashairi ambalo ni lazima lizingatiwe na kila mshairi. Dhamiri yetu katika makala hii ni kutizama rai mbali mbali zinazotolewa na wawakilishi wa makundi hayo mawili yanayozozana na kutoa msimamo wetu na sababu zake.

Kundi la kwanza katika mabishano tunayozungumzia lina watu kama vile K. A. Abedi, S. Chiraghdin, J. M. Mayoka, S. A. Kandoro, A. Abdalla, A. Nabhany, A. Baruwa, R. K. Ruo, A. Gibbe na D. Massamba. Baadhi ya waliomo katika kundi la pili ni F. Topan, E. Kezilahabi, K. K. Kahigi, M. M. Mulokozi na E. Hussein. Katika makala hii kundi la kwanza litajulikana kama 'wana-vina' na kundi la pili kama 'wana-mtiririko.'[2]

Kwa mujibu wa masimamo wa wana-vina, ili kustahiki jina 'shairi' ni lazima utungo utimize masharti yafuatayo: urari wa vina, ulinganifu wa mizani, kujitosheleza kwa kila ubeti, usawa wa idadi ya mishororo katika kila ubeti, muwala au mtiririko mzuri wa habari na kuweza kuimbika. Hatima ya kutimizwa masharti hayo ni utungo wenye umbo kama lifuatalo:

Mwendani sinishitaki, likupatalo nyamaza

Mimi sitokushiriki, wala sitakuuliza

Kulla mtupa tariki, hawati kujipoteza

Asiyetaka kufunzwa, hasalimiki na jambo

Nalikwambiya kitambo, mwendani wangu sikiza
Siteze na mawi mambo, ukanambiya tateza
Leo mwapigana kumbo, kulla wendapo husosa
Asiyetaka kufunzwa, hasalimiki na jambo

Ulijifanya mwekevu, kulla jambo waliweza
Kwa kuaminiya nguvu, akili ukapoteza
Leo yamekuwa wavu, tatizi mekutatiza
Asiyetaka kufunzwa, hasalimiki na jambo

Nalikwambiya latisha, ukapinga tangu mbele
Na leo limekutwesha, vumilia vile vile
Mwiba wa kujitonesha, mtu haambiwi pole
Asoonyeka milele, hasalimiki na jambo.[3]

Kwa jumla hilo ndilo umbo la mashairi ya Kiswahili lijulikanalo vizuri hivi sasa. Hilo ndilo umbo linalotetewa na wana-vina. Kwa mujibu wao utungo usio na umbo kama hilo, kwa sababu ya kutozingatia masharti tuliyotaja, haustahiki kuitwa shairi. Kwa hivyo wana-vina wanakana kwamba utungo kama ufuatao ni shairi:

Ni wakati wa mhanga
Na katika jangwa la anga
Utawala wa giza

Umenyanyasa nyota

Kama maji ya mtungi
Nimo tuli kitandani
Mwili wangu-
        godoroni
Kichwa changu-
        mtoni
Macho yangu-
        darini
Mawazo yangu-
        gudini
Nashawishi usingizi
Bila sauti ya mwendo
Uninyemelee kwa ujuzi
Unigubike gubi mwanana
Yanihame mavune mwilini
Na kunipeperuka machovu
Kutoka mipeto ya akili

Lindini mwa kumbukumbu

Nayakumbuka mahindi-

    yaliyo ghalani

Nawakumbuka panya-

    Walio nyumbani

        - Nyuso nyeusi

        - Tumbo nyeupe

        - Mikia myeusi

Kwa nongonezo azizi

Moyo wangu wanishauri

    Huu wakati wa giza

    Si wa kulegeza maungo

    Katika usingizi

Kwa nadhari thabiti

Napiga shoti

Hadi kwenye meza ya vita

Na kwa vyanda imara

Na moyo wa chuma

Nashika kalamu

Na kwa ndoto ya ushindi

Kuanza mashambulizi mapya

Dhidi ya vikosi vya panya.[4]

Kwa maoni ya wana-mtiririko utungo huo ni shairi, bali kwa mujibu wa wana-vina, badala ya kuwa ni shairi, ni 'mkorogano wa maneno yasiyoimbika.'[5] Wana-vina wanaonelea kwamba tungo za namna hiyo hazina budi kupingwa kwa dhati kwani:

> Kwa Kiswahili, tungo zifuatazo mwendo huo, mizani zake hazitakuwa na kichwa wala miguu. Kanuni zote za ushairi wa kiswahili zitakuwa pindu, vina vitakuwa havijulikani mwanzo havijulikani mwisho, na lugha yenyewe itakuwa chapwa au kuzidi. Na tungo hizi zikikubaliwa kuwa ni mashairi basi ushairi wa Kiswahili utakuwa umeanguka kitakotako.[6]

Kutokana na upinzani wa wana-mtiririko, wana-vina wamejaribu kutetea msimamo wao kwa kutoa madai mbali mbali. Kwa mfano, wanadai kwamba vina na mizani ni utamaduni wa Waswahili na Wabantu kwa jumla na kwamba kuacha matumizi yake katika ushairi kutakuwa ni kuharibu utamaduni huo.[7] Pia wanasema kwamba vina na mizani ndio 'uti' wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili na kwamba vitu hivyo ndivyo hutofautisha ushairi wa Kiswahili na wa lugha nyingine.[8] Inadaiwa pia kwamba umbo la hivi sasa la mashairi ya Kiswahili limefikiwa baada ya maendeleo ya muda mrefu sana na kwamba ni kilelelecha cha ustadi wa utunzi.[9] Dai jingine ambalo limewahi kutolewa ni kwamba vina vina dhima mbali mbali katika ushairi ikiwepo dhima ya kusisitiza maana.[10]

Msimamo wa wana-vina umewastaajabisha sana wana-mtiririko. Kundi la wana-mtiririko lashikilia kwamba si lazima kila shairi liwe na vina na mizani (au sheria kama alivyoziita K.A. Abedi)[11.] Katika utetezi wa msimamo wao, kundi hili linadai kwamba umbo la mashairi halina budi kubadilika. Kuhusiana na suala hili M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi wanasema:

> ---utunzi wa mashairi hauna budi kuwa na uhai kama ilivyo lugha yenyewe

> ya Kiswahili; yaani utunzi wa mashairi hauna budi kubadilikabadilika. Njia nyingine mpya lazima kuvumbuliwa…[12]

Kwa jumla tunaweza kusema kwamba mabishano juu ya umbo la mashairi yametokana na hali ya wana-vina ya kutouelewa ushairi kwa upana wake na sifa zake muhimu. Hali hiyo inajitokeza wazi katika baadhi ya madai yao. Mengi ya madai hayo ni ya kuchekesha. Kwa mfano, baadhi yao wamedai kwamba vina na mizani ndivyo vitu ninavyoutofautisha ushairi wa Kiswahili na wa lugha nyingine. Fasiri ya dai hili ni kwamba tukiona utungo wenye sifa hizo tuwe na hakika kwamba ni shairi la Kiswahili. Tuchukue mfano:

So, so break off this last lamenting kisse,
    which sucks two soules, and vapours both away,
Turne thy ghost that way, and let me turne this
    And let ourselves benight our happiest day,
We ask'd none leave to love, nor will we owe
    Any, so cheape a death, as saying, Goe.
Goe; and if that word have not quite kill'd thee,
    Ease me wih death, by bidding me foe too.
Oh, if it have, let my word worke on mee,
    And a just office on a murderer doe.
Except it be too late, to kill me so,
    Being double dead, going, and bidding doe.[13]

Ikiwa vina na mizani ndizo sifa zinazotofautisha ushairi wa Kiswahili na wa lugha nyingine, basi ni 'wazi' kwamba utungo huu ni shairi la Kiswahili!

Mtaalam mmoja wa kundi la wana-vina, S. Chiraghdin, amewahi kutoa kauli nyingine ambayo pia ni ya kuchekesha. Akizungumzia fikra zitolewazo na washairi, alidai kwamba:

…hapa ndipo mashairi ya Kiswahili yanapokuwa tofauti na ushairi mwingine,

wa Kizungu mathalani, mshairi wa Kiswahili hapo ni mwakilishi wa umma.[14]

Kwa mujibu wa kauli hiyo, washairi wa Kiswahili wanajishughulisha na masuala yanayohusu umma ilhali washairi wa lugha nyingine wanajishughulisha na mambo yasiyohusu umma. Hivyo basi, ushairi wa Denis Brutus, Kim Chi Ha, Agostino Neto, Ernesto Cardinal, David Diop, Betolt Brecht na washairi wengine wasiotumia lugha ya Kiswahili si wawakilishi wa umma. Kwa kushikilia uzi huo wa mambo, mshairi aliyetunga shairi lifuatalo si mwakilishi wa umma:

Only by suffering out the napalm in Beirut

reviving the peasant girl in Vietnam's smile

washing the blood from the streets of

Chalatenango, the Bronx, Santiago, San

Francisco Nortre,

Belfast San Juan

will I be able to sleep

in love

at rest

alert[15]

Nimetoa mifano ya mashairi hayo mawili ya Kingereza ili kukanusha madai kwamba vina na mizani hutofautisha ushairi wa Kiswahili na wa lugha nyingine na kwamba washairi wa Kiswahili pekee ndio wawakilishi wa umma. Nimefanya hivyo kama sehemu ya ufafanuzi wa kauli yangu kwamba mabishano juu ya umbo la mashairi yamezushwa na hali ya wana-vina ya kutomakinika katika masuala ya ushairi. Hiyo ndiyo hali inayowafanya kupinga ushairi usio na vina na mizani.

Mojawapo ya hoja ambazo zimewahi kutolewa kama sababu kubwa ya kupinga ushairi usio na vina ni kwamba:

> Vina ni utamaduni wa Kiswahili na wa Wabantu wengine pia. Shairi lisilokuwa
>
> na vina huwa limekiuka mipaka ya utamaduni ambao ndio mvyazi wa lugha.[16]

Ili kuendeleza mjadala, tuchukulie kwa hivi sana kwamba ni kweli kuwa vina ni utamaduni wa Washahili na wa Wabantu wengine pia. Utetezi huu wa vina hauna mashiko yoyote. Ungekuwa na mashiko katika hali ambapo kitu cho chote kilichomo katika utamaduni ni lazima kiwe kizuri na kwamba kila ukiukaji mipaka ya utamaduni ni jambo baya. Ni ukweli usiohitaji ufafanuzi kwamba kuwemo kwa kitu katika utamaduni hakumaanishi kwamba sharti kitu hicho kiwe kizuri. Pia ni kweli kwamba siyo kila ukiukaji mipaka ya utamaduni huwa mbaya. Hivyo basi, utetezi wa vina kwa kusema kwamba ni utamaduni wa Washahili ni utetezi ambao umejengeka katika msingi potovu wa mdahalo.

Wana-vina wanaposema kwamba vina ni utamaduni wa Waswahili na wa Wabantu wengine wanamaanisha kwamba vina viliibuka vyenyewe kaika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu na wala havikufika pande hizi kutokana na athari za kigeni. Hoja hiyo imepingwa vikali na baadhi ya wana-mtiririko. Kwa mfano, M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi wanasema kwamba:

> Suala la athari za ushairi wa Kiarabu kwenye ushairi wa Kiswahili si
>
> jambo ambalo lahitaji mjadala mrefu kwa vile ni dhahiri sana.
>
> Waandishi wa kwanza wa mashairi ya Kiswahili walikuwa masheikh

> na walimu wa dini waliotaalamika katika lugha ya Kiarabu na Kurani ... kwa kuwa kila kitu cha asili ya Kiarabu kilikuwa ndicho kipimo cha ustaarabu, hata walipoanza kuandika mashairi … walichukulia kuwa ni jambo linalokubalika kuwa shairi lazima liwe na urari wa vina na mizani.[17]

Wana-vina wametoa mifano kutoka fasihi-simulizi ya Kiswahili na lugha nyingine za kibantu ili kutetea kauli yao kwamba vina katika ushairi wa Kiswahili havitokani na athari za Kiarabu.[18] Hata hivyo bado hawajaeleza ni kwa nini msamiati unaohusu sifa nyingi za umbo la hivi sasa la mashairi ya Kiswahili una asili ya Kiarabu.[19]

Suala la asili ya vina na mizani katika Ushairi wa Kiswahili ni muhimu, hususa kwa wale wanaotaka kuitalii historia ya ushairi huo. Hata hivyo suala hilo halina uhusiano wa moja kwa moja na mjadala tunaojishughulisha nao. Kwa maoni yangu, ni makosa kutumia asili ya kitu kama kipimo cha thamani yake. Kuendelea kutumiwa au kutotumiwa vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili kwapaswa kutegemea umuhimu wa matumizi ya vitu hivyo na wala sio asili yake. Kwa maoni yangu, swali la kimsingi kuhusiana na mjadala wa vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili ni: Je, kutumia au kutotumia vina na mizani kunafaidi au kuhasiri vipi ushairi huo? Swali hili bado halijajadiliwa katika mkabala mwafaka. Hebu tulichunguze kwa makini.

Gibbe amedai kwamba vina vina dhima mbali mbali katika ushairi. Dhima hizo ni:

> … kupambanua utanzu wa ushairi… kupamba shairi … kusaidia kumbukumbu … kukuza Kiswahili kwa misingi ya Ubantu … kusisitiza maudhui … [na] … kuhifadhi na kueneza msamiati …[20]

Miongoni mwa dhima hizo ni ile ya ‘kupamba shairi’ pekee iliyo na uzito unaostahiki staha; nyingine zimetiliwa chumvi. Baadhi hata zinapotosha. Hatuhitaji vina ili kuhifadhi na kueneza msamiati. Hatuhitaji vina ili kukuza Kiswahili kwa misingi ya Ubantu. Vina ni sifa ya umbo la nje na umbo la nje halitoshi kutofautisha nyanja moja ya fasihi kutoka nyingine.[21]

Akizungumzia dhima ya kusaidia kumbukumbu, S. Robert alidai kwamba wanafunzi wa madrasa ya El Hazar huko Misri huhitajika kukariri Kurani nzima kama mtihani wa kujiunga na madrasa hayo.[22] Anatoa kauli kwamba jambo hilo linawezekana kwa kuwa Kurani ya Kiarabu ina vina. Kauli hiyo ina dosari kubwa. Ili kuthibitisha kisayansi kwamba wanafunzi hao huweza kukariri Kurani nzima kwa sababu ina vina ni lazima kuwe na kundi jingine la wanafunzi au makundi kadha wa kadha ambayo yameshindwa kuikariri Kurani nzima na ikaonyeswa wazi kwamba mambo mengine miongoni mwa makundi yote yanalingana isipokuwa kwamba kundi la kwanza pekee ndilo lililokuwa na Kurani yenye vina. Bila utaratibu huo wa kisayansi kutekelezwa, hatuwezi kutilia maanani kauli ya S. Robert.

Kutokana na tajriba ya maisha yangu, hakuna kitu cho chote ambacho kimewahi kunibainishia kwamba vina husaidia kumbukumbu. Ng'ano tulizohadithiwa utotoni hazikuwa na vina na mizani. Hata hivyo, wale waliotutambia ng'ano hizo waliweza kuzikumbuka ingawaje baadhi zilikuwa ndefu na zilizochanganya maelezo na nyimbo. Huko Afrika ya Magharibi, hususa Mali na Guinea, kuna watu walio na uwezo wa kuelezea kwa undani historia ya karne kadha wa kadha.[23] Sina habari kwamba vina ndivyo huwezesha jambo hilo kusibu. Niwewahi kusoma mashairi ya aina mbali mbali, yenye vina na mizani na yasiyo na vina na mizani. Sioni kwamba nayakumbuka yale yenye vina kuliko yale yasiyo na vina. Kwa mfano ninakumbuka vizuri sana mshororo mmoja usemao:

> During a history of folly fools rule[24]

Siukumbuki mshororo huo kwa sababu ya vina. Nadhani naukumbuka kwa sababu ya uwezo wake wa kujibu au kujaribu kujibu maswala muhimu juu ya hali ya sehemu mbali mbali za ulimwengu, hususa bara la Afrika. Maswala hayo ni mengi. Ni kwa nini uzuzu umekithiri jinsi ulivyokithiri katika ikulu za Afrika? Itakuwaje Mobutu Sese Seko awape Waamerika uwanja wa kutua ndege zinazobeba silaha za kujeruhi na kuua watu wa Angola? Itakuwaje Jean-Bedel Bokasa atumie fedha chungu-nzima kujitawaza mfalme badili ya kutumia fedha hizo kuinua hali ya maisha ya watu wa Jamhuri ya Afrika ya Kati? Itakuwaje Hastings Kamuzu Banda awe rafiki mkubwa wa makaburu wa Afrika Kusini? Mshororo nilioudondoa hapo juu unajaribu kuyajibu maswali hayo kwa kusema kwamba viongozi wengi wa Afrika ni mazuzu kwa sababu ya historia tenge barani hilo. Nadhani hiyo ndiyo sababu inayonifanya niukumbuke mshororo huo na wala

siyo kwa kuwa mshororo wenyewe umo katika ubeti ulio na vina vya ka,ka,ka, ye; ro,ro,ro, ma au ti,ti,ti,le!

Kuhusiana na dhima ya kusisitiza maudhui, Gibbe anatoa mfano wa shairi lifuatalo:

Siku ya panga kufuta
Mashujaa kwenda kondo
Siku ya kuja matata
Na fadhaa na mshindo
Siku ya watu kuteta
Kufua moyo mfundo
Siku ya nchi kutota
Kwa damu kwenda mkondo
Siku ya kung'ara nyota
Za watenzi na matendo
Na siku ya kujivuta
Wa kati na kando kando
Bora ni kufa kwa vita
Au ni kufa kwa sondo.[25]

Akirejelea maoni ya E. Kezilahabi, A. Gibbe anasema kwamba kezilahabi anadai ya kuwa:

> "Mlio wa –do umewekwa mwishoni… mlio huu unaleta hali ya mkazo
> na mpigo wake unasikika kama nyundo ya mfuaji. Katika ubeti …

> tunaona…mwendo, msukumano na msukosuko.Tunaona watu wanaochomwa panga, tunasikia vishindo vya watu wanaokimbia au kuanguka, tunaona wanateta na mwisho tunaona damu nyingi inatiririka katika mkondo. Hiyo ndiyo picha tunayoipata – picha halisi ya vita".[26]

Kwa upande wake Gibbe anasema kwamba "kwa jumla kina - ndo kinatilia mkazo maudhui ya vita." Maoni hayo ya Kezilahabi na Gibbe yamenukuliwa kwa uchangamfu mwingi na J. M. Mayoka.[27] Ningependa kukanusha kauli kwamba kina cha-ndo kinatilia mkazo maudhui ya vita katika shairi tunalolizungumzia. Kina cha -ndo kikiondolewa kutoka ubeti huo maudhui ya vita yatabaki yale yale yakiwa na uzito ule ule. Kwa wale ambao wanaona ugumu kukubaliana na maoni yangu, niko radhi kuwatolea ithibati. Tunapozungumza juu ya kina cha -ndo tunamaanisha ile hali ya –do kuja mwisho wa kila mstari wa pili katika ubeti uliodondolewa. Hivyo basi, kwa mujibu wa arudhi ya ushairi wa vina, utaratibu huo unapobadilishwa hivi kwamba –ndo haiji mwisho wa mishororo, ubeti huo hautahesabiwa kwamba una kina cha-ndo. Hiyo ndiyo hali tunayoipata tunapobadili mpangilio wa maneno katika mistari mbalimbali ya ubeti huo. Matokeo ni utungo ufuatao:

Siku ya kufuta panga
    Kando mashujaa kwenda
Siku ya matata kuja
    Na fadhaa na mshindo
Siku ya watu kuteta
    Kufua mfundo moyo
Siku ya kutoka nchi
    Kwa kwenda mkondo damu

Siku ya nyota kung’ara

Za matendo na watenzi

Na siku ya kujivuta

Wa kando kando na kati

Bora ni kufa kwa vita

Au ni kufa kwa sondo?

Kimaudhui, sioni kwamba utungo katika hali ya pili unatofautiana na utungo katika hali ya kwanza. Maudhui katika hali zote yanalingana shilingi kwa ya pili. Ingekuwa ni kweli kwamba kuwekwa mwishoni mwa mistari –do kunachangia maudhui kwa sababu ya kuwepo mwishoni mwa mishororo katika hali ya kwanza ya utungo kulingana maudhui katika hali zote mbili za utungo hakungekuwepo.[27]

Huko nyuma tulisema kwamba miongoni mwa dhima za vina zinazotajwa na Gibbe ni moja tu iliyo na uzito unaostahili kuzungumziwa kwa kirefu. Hiyo ni dhima ya kupamba shairi. Ni kweli vina na mizani hupamba shairi. Kwa maoni yangu, kuna masuala mawili pekee ambayo ni muhimu katika mgogoro wa vina na mizani. Masuala mengine yanapachikwa tu bila stahiki yo yote. Suala la kwanza muhimu linahusu swali la iwapo kupanda shairi ni jambo muhimu. Endapo itaonekana kupamba shairi ni jambo muhimu, suala la pili la kimsingi litahusu swali la iwapo vina na mizani ndiyo njia ya pekee ya kupamba shairi au pengine kuna mbinu nyingine ambazo pia zaweza kutekeleza kazi hiyo.

Inakubalika miongozi mwa wataalam wa fasihi kwamba mojawapo ya sifa muhimu za fasihi – ukiwemo ushairi – ni ile hali ya kuwasilisha fikra, hisi, mawazo, tajriba, n.k. kwa lugha inayovutia na kupendeza msomaji au msikilizaji, yaani, umbuji. Kupendeza huko kwa lugha ya fasihi kunatokana na lugha kutumiwa kisanaa katika fasihi. Mojawapo ya sifa za lugha iliyotumiwa kisanaa ni urembo wake ikilinganishwa na lugha ya mazungumzo au maandishi yasiyo ya kifasihi. Hivyo basi kupamba shairi, tamthilia, riwaya au hadithi-fupi ni jambo zuri kwa vile linaipa kazi inayohusika urembo.

Sasa tujiulize ni kwa jinsi gani vina na mizani hupamba shairi? Sidhani kwamba swali hilo limejadiliwa kwa undani na washiriki wa mgogoro wa umbo la mashairi ingawaje humo ndimo lililomo, labda, suluhisho la mgogoro huo. Urari wa vina ni kurudiwarudiwa sauti au kundi la sauti mwishoni mwa vipande vya mishororo. Ulinganifu wa mizani ni kurudiwarudiwa idadi ileile ya mizani katika mishororo ya shairi. Kwa usemi tofauti, ulinganifu wa mizani ni usawa wa urefu wa mishororo ya shairi. Kipimo cha urefu huo huwa silabi au mapigo katika matamshi. Marudiorudio hayo ya sauti au kundi la sauti na idadi ileile ya mapigo katika matamshi (au mizani) kunalipa shairi mdundo. Mdundo wa shairi, kama ilivyo midundo katika tanzu nyingine za sanaa kama vile muziki na ngoma, huvuta, hupendeza na hutumbuiza hisia za binadamu. Lakini je, hakuna namna nyingine ya kujenga mdundo katika shairi badala ya kutumia vina na mizani?

Mdundo ni kule kurudiwarudiwa kitu kilekile au kurejelewa utaratibu fulani. Mdundo katika ngoma hutokana na kule kurudiwa utaratibu wa mwendo wa viungo vya mwili kama vile miguu, kiuno, mikoni au kichwa. Mdundo katika muziki hupatikana kwa kurejelewa mpangilio maalum wa noti. Mwendo wa miguu, kiuno, mikono au kichwa katika ngoma ni wa namna nyingi. Vivyo hivyo mpangilio wa noti katika muziki. Hiyo ndiyo sababu midundo ya ngoma mbalimbali hutofautiana. Hiyo ndiyo sababu kila uchao kuna nyimbo mpya za muziki na kila mojawapo ya nyimbo hizo huwa na mdundo (yaani, lahani au tuni) mahususi tofauti na midundo ya nyimbo nyingine. Uwezekano huo wa kuunda midundo ya namna mbalimbali upo pia katika ushairi. Tunaweza kujenga mdundo wa shairi katika viwango mbalimbali vya lugha ikiwa ni pamoja na fonolojia, mofolojia, sarufi au mantiki. Katika kila mojawapo ya viwango hivyo vya lugha, kuna uwezekano wa midundo kadhaa. Wana-vina wamepuuza midundo ya viwango vingine vya lugha isipokuwa kiwango cha fonolojia. Vina na mizani (yaani sauti na silabi) ni sifa za kifonolojia. Vina na mizani ni njia mojawapo tu ya kujenga mdundo katika mashairi na si lazima kutumia sifa hizo ili kujenga mdundo katika shairi.

Ili kuthibitisha kauli kwamba kuna njia kadha wa kadha za kuundia mdundo katika ushairi mbali na vina na mizani, tutazame utungo ufuatao:

Majonzi na simanzi!

Shakawa na mashaka!

Ai chawa nyweleni

Na kunguni kitandani

Na mende mekoni

Na panya ghalani

Na nguchiro kizimbani

Na nyegere mzingani

Na fuko kondeni-

Ghamu!

Dhiki na zahama

Zahama na ndoto

Ndoto na makungu

Makungu ya kesho –

Nuru![28]

Utungo huo, ambao kwa maoni yangu na ya wanamtiririko wengine ni shairi na una mdundo ulio wazi. Ingawaje hivyo, mdundo huo hautokani na matumizi ya vina na mizani. Mdundo huo umejengeka sio katika kiwango za fonolojia, bali mofolojia, sarufi na mantiki. Tutazame mfano mwingine:

Kwa sauti ya hati

Wabunge walihukumu:

Baada ya pete, mwanamke

Ni kwembe,

    Ni membe,

        Ni njiwa

Asakini tanzuni mwa miti;

Ni kuro,

    Ni tohe,

        Ni swara

Asakini wandani mwa nyika

Ni mhanga,

    Ni nungu,

        Ni fuko

Asakini chini ya ardhi

Ni pandu,

    Ni tonzi

        Ni tafi

Asakini chumvini mwa bahari[29]

Hapa tena tuna utungo usio na vina na mizani lakini ambao una mdundo unaoonekana kwa macho, sikuambii kuwa dhahiri katika fahamu.

Sasa tukusanye pamoja mambo yanayohusu masuala ambayo tulisema ni muhimu kuhusu mjadala wa umbo la mashairi. Tumeona kwamba urembo ni mojawapo ya sifa za lugha ya fasili. Pia tumeona kwamba vina na mizani hurembesha au hupamba shairi kwa kulipa mdundo. Jambo la mwisho tulilogundua ni kwamba kuna njia nyingine za kujenga mdundo katika shairi mbali na vina na mizani. Ni kwa nini basi wana-vina wanang'ang'ania kwamba ni lazima shairi liwe na vina na mizani? Vitu hivyo si vya lazima katika ushairi. Ukweli huo unafahamika katika jamii nyingine za ulimwengu. Hiyo labda ni mojawapo ya sababu jamii zilizokuwa zikitumia vina na mizani katika ushairi nyakati za nyuma, kama vile Waarabu, Wajerumani, Waingereza, Warusi, zimeacha kutilia mkazo sifa hizo katika ushairi.

Pengine yafaa niongezee kusema vina na mizani hutupa hali ya chini ya urembo katika mashairi. Mdundo unaotokana na vina na mizani, kama ilivyo hivi sasa katika ushairi wa Kiswahili, ni mdundo uliokithiri na wa kutabirika. Hivyo basi, badala ya kupendeza hisia za kila msikilizaji unazifanya hisia za baadhi ya wasikilizaji kukinai hasa wanapokutana nazo kipande baada ya kipande, mshororo baada ya mshororo na shairi baada ya shairi!

Kabla ya kuliacha suala la mdundo katika ushairi, ningependa kutaja kwamba mdundo ni sifa mojawapo tu ya urembo au pambo katika mashairi. Zipo sifa nyingine nyingi. Kwa sababu hiyo, siyo lazima kila shairi liwe na mdundo ulio wazi ili livutie hisia za msomaji au msikilizaji. Kuna sifa nyingine mbalimbali za kifasihi ambazo huchangia urembo wa mashairi. Kwa mfano shairi laweza kuvutia kutokana na matumizi mazuri ya jazanda, tashibihi, tashihisi, balagha, chuku na tamathali za usemi nyinginezo. Hali hiyo inamaanisha kwamba siyo lazima mshairi ajishughulishe na mdundo katika kila shairi.

Natumai nimezungumza vya kutosha kuhusu vina na mizani. Vina na mizani ni baadhi ya masharti ambayo wana-vina wanashikilia kwamba ni lazima yatimizwe ili utungo ustahiki jina 'shairi'. Tumeonyesha kwamba masharti hayo mawili siyo lazima yatimizwe na mshairi. Ningependa kuzungumzia, kwa kifupi, masharti yaliyosalia, yaani: kujitosheleza kwa kila ubeti, muwala, idadi sawa ya mishororo katika kila ubeti, na kuimbika kwa shairi.

Muwala au mtiririko mzuri wa habari ni muhimu katika mambo kama vile mazungumzo ya kawaida, kazi za fasihi, magazeti na hotuba. Muwala siyo sifa ya ushairi wa vina pekee,

unapatikana pia katika ushairi wa mtiririko bora tu shairi liwde limeandika na mshairi ambaye amemakinika katika uandishi. Kwa vile jambo hilo siyo inayopatikana katika mashairi na mizani pekee, sioni kwamba ni suala la kujadiliwa katika makala hii.

Wana-vina wanasema ni lazima kila ubeti ujitosheleze. Kama lilivyo sharti la muwala, msimamo huu hauhitaji mjadala hasa ikiwa ‘kujitosheleza’ kutafasiriwa kuwa na maana ya kukamilika katika uendelezaji wa sehemu ya dhana, fikra, tajriba au rai. Hiyo ndiyo hali inayotajariwa katika beti za mashairi na aya za maandishi ya nathari. Hiyo ni hali inayopatika siyo tu katika ushairi wa vina na mizani bali pia katika ushairi wa mtiririko.

Nyakati za nyuma washairi wa lugha nyingi za ulimwengu walikuwa wakitumia idadi sawa ya mishororo katika beti za mashairi yao, jambo ambalo lingali likiendelea katika ushairi wa Kiswahili.[30] Jambo hilo lilizipa beti ukubwa sawa. Kulingana kwa ukubwa wa beti unayapa mashairi mdundo kwani, kama tulivyoona huko nyuma, mdundo hutokana na kurejelewa kwa sifa fulani katika kazi inayohusika. Kwa hivyo, kwa jumla, tunaweza kusema kwamba ushairi wa vina na mizani katika Kiswahili unapata mdundo wake kutokana na sifa tatu: urari wa viva, ulinganifu wa mizani na idadi sawa ya mishororo katika beti.

Tayari tumesema kwamba si lazima mshairi ajishughulishe na mdundo katika shairi. Pia tumesema kwamba kuna njia mbalimbali za kuundia mdundo katika shairi na kwamba hatuoni sababu ya mojawapo ya njia hizo kufanywa kuwa lazima kwa kila mshairi. Hilo ndilo jambo watunzi wa ushairi wa vina na mizani na mashabiki wao wanalong’ang’ania – kwamba ni lazima kila shairi la Kiswahili liwe na mdundo na kwamba mdundo huo ujengeke kutokana na urari wa vina, ulinganifu wa mizani, na idadi sawa ya mishororo katika beti.

Sioni jambo la kuwafanya watu wavutane kuhusu beti kutokuwa na ukubwa sawa. Ingelikuwa kila wazo linalingana kwa uzito na kila wazo jingine au kila dhana ina upana sawa na wa kila dhana nyingine, lingelikuwa jambo la kutarajiwa kwamba katika shairi lenye beti kadhaa kila ubeti utakuwa na idadi sawa ya mishororo. Lakini hivyo sivyo hali ya mambo ilivyo. Kunapokuwa na dhana kadhaa aghalabu dhana hizo huwa na uzito, upana au umuhimu usiolingana. Kwa sababu hiyo, sura katika vitabu hazilingani kwa kurasa na aya hazilingana kwa idadi ya sentensi. Kunapokuwa na hoja kadhaa za kujadiliwa katika mkutano, muda unaotumiwa

kushugulikia kila mojawapo ya hoja hizo aghalabu hutofautiana. Vivyo hivyo, fikra katika akili ya mshairi hutofautiana kwa uzito, upana, kina au umuhimu. Huo ndio ukweli unaojitokeza katika ushairi unaopingwa na wana-vina, yaani, ushauri wa mtiririko. Katika ushairi huo, ukubwa wa ubeti hutegemea kile kinachozungumziwa, kufafanuliwa, kujadiliwa, kufasiriwa au kudadisiwa katika ubeti huo na wala ukubwa hautegemei kanuni zisizoongozwa na hali mahususi ya ubeti unaohusika. Jambo hili haliharibu shairi kwa namna yo yote bali husaidia katika uendelezaji mzuri wa maudhui.

Tulichunguze sharti la kuimbika kwa mashairi. Isipokuwa idadi ndogo ya mashairi ambayo huimbwa redioni au pengine shuleni wakati watoto wanapowakaribisha wazazi au kuwatumbuiza viongozi na vilevile katika tamasha za muziki ambapo kunakuwa na sehemu ya kuwasilisha mashairi, siku hizi mashairi hutungwa ili yachapishwe katika magazeti, majarida na vitabu. Je, kuna maana gani kushikilia kwamba shairi ambalo halikusudiwi kuimbwa ni sharti liimbike? Baada ya kuchapishwa, mashairi husomwa darasani, maktabani, katika vyumba vya mitihani, nyumbani na kwingineko. Isipokuwa darasani, ambako pengine shairi litasomwa kwa sauti kabla ya kuchambuliwa na mwalimu na wanafunzi, aghalabu mashairi husomwa kwa ughaibu. Katika jamii ya Waswahili mashairi yaliimbwa katika sherehe za gungu.[32] Darasa, maktaba au chumba cha mtihani si kumbi za gungu! Mazingara ya ushairi wa Kiswahili yamebadilika kwa sababu ya kuenea kwa Kiswahili na kubadilika nyakati.[33] Ushairi huo hauna budi kuoana na hali hiyo mpya. Kuoana kwa sanaa na nyakati mpya si jambo geni katika ulimwengu wa sanaa bali ndio uhalisi wa utanzu wo wote ule wa sanaa ulimwenguni. Sanaa hubadilika kuambatana na mabadiliko ya jamii. Ni jambo la kushangaza kwamba ukweli huo bado haujafahamika miongoni mwa 'wataalam' wa ushairi.

Wana-vina wanapozungumzia kuimbika kwa mashairi wanamaanisha mashairi yawe na mizani. Hivyo basi, sharti la kuimbika linafungamana na lile la ulinganifu wa mizani ambalo tulilijadili huko nyuma. Inaonekana wana-vina wanaamini kwamba utungo usio na ulinganifu wa mizani hauwezi kuimbika. Jambo hilo si kweli hata kidogo. Ni kweli kuna kundi dogo la nyimbo ambazo zina mizani.[34] Hata hivyo, nyimbo nyingi ulimwengu hazina mizani na bado zinaimbika. Nyimbo za Daudi Kabaka, Fadhili Williams, Simba wa Nyika, Les Mangelepa, Mariam Makeba, Angelique Kidjo, Salif Keita, Bob Marley na Don Williams hazina ulinganifu wa mizani. Hata

hivyo, zinaimbika vizuri sana. Anayetaka kuyaimba mashairi atayaimba hata yasipokuwa na mizani, bora tu awe anaielewa sanaa ya uimbaji!

Ningependa kuhitimisha makala hii kwa kukanusha dai la wana-vina kwamba ushairi wa mtiririko utaharibu na kuangamiza sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Turejee tena maoni ya S. Chiraghdin kuhusu ushairi wa mtiririko. Mwana-vina huyo anahofu kwamba:

> Kwa Kiswahili, tungo zifuatazo mwendo huo, mizani zake hazitakuwa na kichwa wala miguu. Kanuni zote za ushairi wa Kiswahili zitakuwa pindu, vina vitakuwa havijulikani mwanzo havijulikani mwisho, na lugha yenyewe itakuwa chapwa au kuzidi. Na tungo hizi zikikubaliwa kuwa ni mashairi basi ushairi wa Kiswahili utakuwa umeanguka kitakotako.

Ushairi wa mtiririko hautangusha ushairi wa Kishwahili kitakotako bali utausukuma mbele kufuatana na mwendo wa nyakati. Hautaua sanaa yake bali utaihuisha. Ni kweli kwamba urari wa vina na ulinganifu wa mizani ni sifa ambazo pengine zitaangamia. Hata hivyo kuangamia kwa sifa hizo hakutakuwa na madhara yo yote katika ushairi wa Kiswahili kwani mambo hayo si ng'arange ya mti wa ushairi bali ni majani yanayoninginia tanzuni. Majani huota yakakua na hatimaye kupukutika na kuanguka chini ya mti na kugeuka masakasaka. Yanapoota, huota kwenye mti ambao tayari upo, yanapokauka na kupukutika huacha mti huo ukiendelea kukua na kusimama wima kwenye uhimili wa mizizi na shina lake. Hivyo ndivyo hali ilivyo katika ushairi na tanzu nyingine za sanaa. Sifa za kijuujuu huzuka, zikashangiliwa na wasanii na hatimaye kutoweka. Kwamba ukweli huo utasibu katika ushairi wa Kiswahili si jambo la kustaajabisha au la kutotarajiwa.

Badala ya ushairi wa mtiririko kuuangusha ushairi wa Kiswahili, utaupanua, kuusambaza na kuuimarisha. Wazungumzaji wa Kiswahili ambao wamekuwa na ilhamu ya kutunga na ambao wangependa kuwasilisha fikra zao kwa ushairi lakini wakawa ama wanatishika na umbo la kulazimishwa la mashairi ya Kiswahili au kupuuza ushairi wenye vina na mizani kwa kusema

kwamba ni “utamaduni wa pwani”, sasa wataweza kuchangia ukuzaji wa ushairi wa Kiswahili. Tutakuwa na watunzi siyo tu kutoka Pate, Lamu, Mombasa na Tanga bali pia kutoka Lodwar, Nyahururu, Mbale, Mwanza na, labda, Bayreuth, Naples na London! Hayo yatakuwa siyo tu maendeleo ya ushairi wa Kiswahili bali pia ukuzaji na utukuzaji wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Badala ya ushairi wa mtiririko kuangusha ushairi wa Kiswahili kitakotako, pingamizi na vikwazo vya kukuza na kuendeleza Kiswahili ndivyo vitakavyoanguka kitakokitako. Hofu ya J. M. Mayoka ambayo inamshawishi kuonya:

> … hatuwezi kuvumilia kuona amali yetu aali tuliyoirithi itiwe kitanzi na hatimaye vizazi vijavyo vije vibaki na tungo mkorogovyo kama kwamba bora wa Kiswahili[35]

ni hofu isiyo na msingi wo wote. Ushairi bora si vina na mizani!

Suala la ushairi wa Kiswahili kuangamizwa na ushairi wa mtiririko na uvyazi wa mitindo mipya laonekana limewatia wasiwasi sana wana-vina wengi. Tumemnukuu S. Chiraghdin na J. M. Mayoka. Wasiwasi hiyo pia inadhihirika wazi katika anwani ya makala ya A. Abdalla inayoitwa “Ushairi wa Kiswahili na Uhuishwe, Usiuliwe” inayozungumzia umbo la mashairi.[36] Kwa upande wake, R. K. Ruo anapiga yowe la hofu akisema:

> Ushairi wa Kiswahili umo katika hatari ya kuharibiwa au hata kuangamizwa na wachache waliozuka baina ya mwaka wa 1960 na 1970. Baadhi ya watunzi hao wafahamu neno ushairi tu bali hawajui ushairi ni fani gani na una asili ya namna gani na jinsi gani asili inavyofungamana na fani hii iliyo na tanzu kadha.[37]

Ninakubaliana kabisa na R. K. Ruo kwamba ipo hatari ya kuharibiwa na kuangamizwa. Hata hivyo, hatari hiyo haihusu hata chembe ushairi wa Kiswahili. Kile ambacho kimo katika hatari ya kuharibiwa na kuangamizwa na ambacho ningependa kuona kikiharibika na kuangamia ni fikra finyu na potoshi kuhusu ushairi za wanaopinga miundo mpya katika ushairi wa Kiswahili.

Chambilecho Kiswahili: HAMUWEZI KWIMA LIUSHALO WIMBO UNGAMA. Tayari wimbi la Ungama laparamia mkoko, miamba na viumbe!

TANBIHI

1. Marejeo mengi juu ya suala hili yanapatika katika J. M. Mayoka (1984): *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka* na katika M. M.Mulokozi na K. K. Kahigi (1979): *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.*

2. Istilahi 'mtiririko' niliyoitumia katika jina 'wana-mtiririko' imewahi kutumiwa na waandishi wengine, kwa mfano M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi (1979), ikimaanisha ushairi usiozingatia kaida za ushairi wa vina na mizani.

3. Shairi la 'Asiyetaka kufunzwa' katika A. Nassir (1974): *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo.*

4. Shairi langu liitwalo 'Vita Dhidi ya Panya' lililochapishwa katika diwani ya *Mchezo wa Karata* baada kufanyiwa mabadiliko.

5. Katika *Sheria za kutunga Mashairi na Diwani ya Amri,* K. A. Abedi anasema:

    > Shairi au utenzi ni wimbo. Hivyo kama shairi haliimbika, halina maana. Kwani ingefaa asiyeweza kutunga mashairi sawasawa aeleze fikira zake kwa maelezo ya desturi kuliko kujitia ndani ya mkorogano wa maneno yasiyoimbika.

6. Kauli ya S. Chiraghdin katika utangulizi wa *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo.*

7. Katika *Mgogoro wa Ushairi na Ushairi na Diwani ya Mayoka J. M. Mayoka,* mwandishi anasema:

    > Vina ni utamaduni wa Kiswahili na wa Wabantu wengine pia. Shairi lisilokuwa na vina huwa limekiuka mipaka ya utamaduni ambao mvyazi wa lugha.

8. Katika makala yake iitwayo 'Vina na Mizani ni Uti wa Ushairi wa Kiswahili iliyochapishwa katika *Lugha Yetu, Na. 9.*' J. M. Mayoka anaelezea kwamba:

> Suala la ushairi wa Kiswahili kuwa na vina na mizani limejadiliwa kwa muda mrefu sasa. Na kweli ya mambo ni kwamba vina na mizani ndiyo uti wa Ushairi wa Kiswahili. Hivyo ndivyo vitu vinavyoutofautisha ushairi huu na wa lugha nyingine.

9. Dai la J. M. Mayoka katika *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka.*
10. _Dai la A. G. Gibbe katika makala yake iitwayo "Vina" katika Ushairi wa Kiswahili'.
11. Kitabu cha K. A. Abedi kinachozungumzia mbinu za utunzi kina anwani ya *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.*
12. Maoni ya M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi katika utangulizi wa *Mashairi ya Kisasa.*
13. Shairi la Jonne Donne katika *The Metaphysical Poets.*
14. Maoni ya S. Chiraghdin katika utangulizi wa *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo.*
15. Shairi la M. Randall katika *A Poetry of Resistance: Selected Poems and Prose from Central America.*
16. Tizama 7 hapo juu.
17. Maoni ya M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi katika *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.*
18. Baadhi ya mifano hiyo imetolewa na J. M. Mayoka katika *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka,* A. G. Gibbe katika '"Vinaa" katika Ushairi wa Kiswahili', na R. K. Ruo katika 'Suala la Ushairi wa Kiswahili: Mtazamo Mwingine'.
19. M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi wanaamini kwamba vina na mizani katika Ushairi wa Kiswahili ni sifa ambazo zimetokana na athari za ushairi wa Kiarabu. Huo ndio msimamo

wao katika Kunga za Utunzi na Diwani Yetu. Wanajaribu kuliimarisha dai lao juu ya jambo hili kwa kusema:

> Msamiati wenyewe unaotumika, shairi, ubeti, mizani, hamziya, tasmit, takhmis, tathlitha, tarbia, n.k. ni wa Kiarabu.

Kuhusu maoni zaidi juu ya suala hili tizama makala ya M. M. Mulokozi iitwayo 'Revolution and Reaction in Swahili Poetry' katika *Kiswahili Tol. 45/2.*

20. Tizama makala yake ya '"Vina"katika ushairi wa Kiswahili'.

21. Upo uwezekano wa kwandika riwaya, tamthilia, insha, n.k. kwa kutumia vina.

22. Madai hayo yamenukuliwa katika '"Vina" katika Ushairi wa Kiswahili.'

23. Kitabu cha *Sundiata: An Epic of Old Mali* kilichoandikwa na D.T. Niane kimetokana na masimulizi ya namna hiyo.

24. Mshororo wa shairi la 'London Calling' katika *Wordloom 1: A New International Literary Magazine.*

25. Shairi la S. Robert liitwalo 'kufua Moyo'

26. Tizama makala ya '"Vina" katika Ushairi wa Kiswahili.'

27. Sikusudii kumaanisha kwamba hakuna sauti zinazoweza kuchangia maana katika shairi. Kuna kundi la sauti ziitwazo 'onomatopea' ambazo milio yake hulingana na mambo mbali mbali duniani. Mashairi anaweza kutumia sauti hizo anapozungumzia mambo hayo. Tizama M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi (1979:32) na R. Antilla (1972)

28. Shairi langu liitwalo 'Ghamu' katika diwani ya *Mchezo wa Karata*

29. Shairi langu liitwalo 'Baada ya Pete' .

30. Nyakati za nyuma washairi wa Kilatini, Kiyunani, Kiajemi, Kiarabu, Kifaransa, Kirusi, Kijerumani, na Kiingereza, kwa mfano, walitunga mashairi yaliyokuwa na vina, mizani na idadi sawa ya mishororo katika kila ubeti. Jamii hizo tayari zimeacha kung'ang'ania

sifa hizo katika ushairi. Badala yake washairi wanazingatia ubunifu kwa maana yake pana, ukiwemo uvyazi wa sifa mpya katika umbo la mashairi.

31. Uimbaji wa mashairi katika sauti ya Kenya ni jambo la kuhuzunisha sana kwa yo yote anayeelewa sanaa ni nini. Mwimbaji wa mashairi hayo hutumia mahadhi yale kwa yale kuliimba shairi lolote lile liwe ni la shangwe ya harusi au usononi wa talaka, faraja ya fanaka au simanzi ya ajali, furaha ya kupata mtoto au ghamu ya kufiwa na mama. Kila shairi hulazimishwa katika mahadhi hayo hayo ambayo huwa tayari yameamuliwa hata kabla ya kusoma shairi likaloimbwa. Hivyo basi katika uimbaji huo hakuwi na uhusiano wa moja kwa moja baina ya mahadhi na maudhui ya shairi, jambo ambalo ni la lazima iwapo shairi litawasilisha ujumbe wake kikamilifu iwezekanavyo.

32. Zamani washairi waliyaimba mashairi yao katika sherehe za gungu. Tizama M. H. Abdulaziz (1979: 50-51)

33. Ni vigumu kujua kwa hakika idadi ya wazungumzaji wa Kiswahili. Hata hivyio, iwapo tutahesabu pia watu walio na uwezo wa kukitumia kwa mawasiliano ya kadri, tunaweza kuikisia idadi hiyo kuwa takribani watu milioni sabini na tano. Watu hao wamesambaa katika eneo kubwa la Afrika zikiwemo nchi za Kenya, Tanzania, Somalia, Uganda, Burundi, Rwanda, Zaire, Malawi, Zambia, Msumbiji na Ngazija.

34. Kwa mfano nyimbo za taarabu.

35. Katika *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka.*

36. Makala hiyo imetajwa katika *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.*

37. Katika makala yake iitwayo ‘Suala la Ushairi wa Kiswahili: Mtazamo Mwingine.’

MAREJEO


1. M. H. Abdulaziz (1979) *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Verse.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

2. K. A. Abedi (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi East African Literature Bureau.

3. T. Baybars (1981) 'London Calling.' Katika *Wordloom 1: A New International Literary Magazine.*

4. H. Gardner (ed) (1972) *The Metaphysical Poets* Harmondsworth: Penguin Books Ltd.

5. A. G. Gibbe (1981) '"Vina" katika Ushairi wa Kiswahili.' Makala iliyotolewa katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam.

6. S. A. Kandoro (1983) 'Hatua mbalimbali za Kubuni na Kutunga Shairi la Kiswahili' Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi.* Dar-es-Saam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

7. E. Kezilahabi (1974) Kichomi. London: Heinemann Educational Books Ltd.

    ____________________ (1983) 'Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili' katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

8. J. Knappert (1979) *Four Centuries of Swahili Verse:* London: Heinemann Educational Books Ltd.

9. D. P. B. Massamba (1983) ‘Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili’ katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III:* Fasihi Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

10. J. M. Mayoka (1977) ‘Vina na Mizani ni Uti wa Ushairi wa Kiswahili’ katika Mulika Na 9.

11. ____________ (1984) *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka.* Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.

12. K. wa Mberia (1997) *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marima Publications Limited. (Wakati wa kuandika makala hii shairi bado halijachapishwa

13. M. Mohamed (1977) *Malenga wa Mrima.* London: Oxford University Press.

14. M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi (1977) *Mashairi ya Kisasa.* Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.

15. M. M. Mulokozi (1975) ‘Revolution and Reaction in Swahili Poetry.’ Katika *Kiswahili, Tol. 45/2.*

16. M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi (1979): *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.

17. A. Nassir (1974) *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo.* Nairobi: Oxford University Press.

18. M. Randall (1984) *A Poetry of Resistance: Selected Poetry and Prose from Central America.* Toronto: Participatory Research Group; Canadian Action for Nicaragua; and the International Women’s Day Committee.

*19.* R. K. Ruo (1983) 'Suala la Ushairi wa Kiswahili: Mtazamo Mwingine' katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi.* Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

---

Makala hii ilitolewa katika Semina ya Walimu, Idara ya Ismu na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi, mnamo tarehe 22 Aprili 1987. Imefanyiwa marekebisho madogo hasa ya kimtindo.